**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA PWANI MH. EVARIST NDIKILO KWENYE KIKAO CHA TATHIMINI YA MKATABA WA LISHE KATIKA MKOA WA PWANI UKUMBI WA MKUU WA MKOA TAREHE 14 APRILI, 2021**

- ***Katibu Tawala Mkoa***
- ***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya***
- ***Viongozi wa Dini,***
- ***Makatibu Tawala Wasaidizi (M),***
- ***Makatibu Tawala wa Wilaya***
- ***Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri***
- ***Watendaji ngazi ya Mkoa na Halmashauri,***
- ***Mabibi na Mabwana.***

***Habari za asubuhi***

***Ndugu washiriki;***

Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na hatimaye kutukutanisha kwa shughuli hii muhimu. Poleni na hongereni kwa majukumu mbalimbali ya kulijenga taifa letu.

Tumekutana hapa leo kwa ajili ya kufanya tathmini ya tatu ya nusu mwaka ya utekelezaji wa mkataba wa lishe ngazi ya Mkoa. Ikumbukwe kuwa, Mkataba wa lishe ulisainiwa tarehe 19 Desemba, 2017 baina ya WN OR – TAMISEMI na Wakuu wa Mikoa yote nchini. Mwaka 2019 katika kikao cha pili cha kutathmini utekelezaji wa mkataba wa lishe ngazi ya taifa lilitolewa agizo na Serikali kuwa kikao hiki kifanyike kila nusu mwaka katika ngazi ya Mikoa. Tumetekeleza kwa kufanya kikao kwa nusu mwaka ya Julai –Desemba mwaka 2019/2020 katika Mkoa wa Pwani. Na sasa tunaendelea kutekeleza kwa kufanya kikao cha tatu cha nusu mwaka cha Julai - Disemba 2020.

Karibuni sana.

*Ndugu washiriki;*

Ni dhahiri kuwa, lishe bora katika jamii ni kichocheo cha maendeleo endelevu katika nyanja zote na hasa ya viwanda, afya, kilimo, Elimu, biashara, uchumi, nk. Hivyo ni pale tu ambapo athari za lishe duni au utapiamlo zitakapodhibitiwa au kutokomezwa ndipo malengo ya maendeleo katika nyanja hizi yataweza kufikiwa kwa ufanisi. ***Hali ya udumavu kwa Mkoa wetu ni 23.8% ukilinganisha na ule wa Taifa 30.1% (TNNS, 2018). Tafsiri yake ni kuwa katika watoto 100 wenye umri chini ya miaka mitano watoto 24 wamedumaa na hawana uwezo wa kufundishika na hata kuinua uchumi wa familia na taifa kwa ujumla.***

*Ndugu washiriki;*

Katika kikao hiki tutaona Tathmini ya Utekelezaji wa Mkataba wa Lishe kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2020 ulivyotekelezwa katika ngazi ya Halmashauri zote tisa. Hali ya utekelezaji **hairidhishi** hususani katika kiashiria kifuatacho:-

i. **Utoaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za lishe.**
   Utoaji wa fedha ambazo ni kutoka mapato ya ndani ambayo ni kiasi cha **sh. 1,000** kwa kila mtoto kwa mwaka umeboreka kwa Halmashauri sita ambazo zimetoa zaidi ya asilimia 90 ya kisasi cha fedha kilichopangwa.
   Halmashauri mbili za Kibaha Mji na Kibiti wametoa kwa aslimia 79.1 na 58.5 ya fedha zilizopangwa mtawaliwa ‘’respectively ‘’.
   Halmashauri ya **Mafia** hali ya utoaji wa fedha zilizopangwa hairidhishi kabisa kwani ni asilimia **28.8** tu ya fedha iliopangwa ilitolewa kwa utekelezaji wa afua za lishe. Hali hii imepelekea Mafia kushindwa kutekeleza viashiria vinne kwa ufanisi wa juu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mafia, utupatie sababu za kushindwa kutoa angalau asilimia 50 ya fedha zilizopangwa. Kwa kweli Mafia inashusha ufanisi wa utekelezaji mkataba wa lishe ngazi ya Mkoa.

Aidha, zipo jitihada katika utekelezaji wa mkataba na inaridhisha hasa kwa Halmashauri za Kisarawe na Mkuranga. Tunawapongeza sana. Mafanikio hayo ni dhamira ya dhati waliyonayo watendaji na wasimamazi wa suala hili.

Baada ya kuona hali halisi kupitia kikao hiki Wajumbe watajadili hali hiyo na tutaweka maazimio kwa viashiria ambavyo ufanisi wake ni wa chini. Maazimio hayo yalenge ufanisi zaidi katika utekelezaji wa mkataba. Kwa kufanya hivi tutapunguza hali duni ya lishe katika jamii yetu. Lakini pia tukumbuke kuwa suala hili lina ushindani Kitaifa si vyema kila tunapokutana Mkoa wetu unakuwa nyuma **haipendezi.**

Niwapongeze kidogo kwa mafanikio tuliyoyapata katika kikao cha kitaifa kilichofanyika Januari mwaka huu. Mkoa wetu ulikuwa wa tano kati ya mikoa yote 26. Ufanisi huu usitufanye tukaacha kuongeza juhudi katika utekelezaji wa afua za lishe bali iwe chachu ya kufanya vizuri Zaidi.

***Ndugu washiriki;***

Jambo la msingi ambalo sote tunapaswa kulifahamu ni kwamba lishe duni ni hatari Zaidi hasa kwa Wanawake Wajawazito, Watoto wachanga na wadogo katika jamii, kwani athari zake ni kubwa sana na hata kusababisha vifo vya akina mama na watoto.

Lishe duni pia husababisha kinga ya mwili kuwa duni. Hivyo mwili hushindwa kupambana na vimelea vya magonjwa mbalimbali. Ili kupunguza gharama kubwa za matibabu ni muhimu kila kaya kujiunga na mfuko wa bima ya afya ya jamii (CHF ilioboreshwa). Hadi sasa hali ya usajili hairidhishi kabisa. Jumla ya kaya 10,038 (5.1%) zimejiunga na CHF iliyoboreshwa kati ya kaya 294,634 kimkoa.

Kuhudhuria kwenu katika kikao hiki ni fursa ya kuboresha Usimamizi wa Utekelezaji wa Mkataba wa Lishe katika Halmashauri zetu sambamba na kuinua kiwango cha usajili wa kaya kwenye ICHF. Tusikilize na tushiriki

vizuri katika mada zitakazowasilishwa ili kupata kujipanga zaidi kuhusu utekelezaji wa Mkataba huu na kuinua usajili wa ICHF.

**Hitimisho**,

Naomba nimalizie kwa kuwashukuru tena nyote mlioshiriki katika maandalizi ya kikao hiki na wajumbe niwatakie uchangiaji wa mawazo ***ili tuweze kutatua changamoto za utekelezaji duni kwa viashiria vilivyobainika.***

**Sasa natamka kikao hiki kimefunguliwa rasmi**

*Asanteni sana kwa kunisikiliza!!!*